Shirika la Kazi Duniani
Mpango wa Kimataifa unaohusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi

# UKIMWI na haki za msingi katika mahali pa kazi

*UKIMWI unatishia haki za msingi katika ulimwengu wa kazi. Kuanzia kutokuwa na ubaguzi wowote katika kuajiri hadi kuondosha umasikini kupitia upatikanaji wa kazi, UKIMWI unahatarisha kanuni za msingi za Shirika la Kazi Duniani kuhusu usawa na haki za jamii, pamoja na kazi yenye manufaa na kuheshimika katika mazingira ya uhuru, usawa, usalama na heshima ya utu wa mtu.*

## Athari kwa haki za msingi katika mahali pa kazi

- UKIMWI unaathiri haki za msingi katika mahali pa kazi na katika jamii kwa ujumla. Ubaguzi unaofanywa kwa misingi ya UKIMWI unafanya hali ya ukosefu wa usawa, kwa mfano kwa misingi ya kijinsia au ukabila iliyopo sasa katika jamii, kuwa mbaya zaidi. UKIMWI unatengeneza mazingira ya lawama na kutojithamini ambako kunadhoofisha jitihada za kukabili janga hili mahali pa kazi na katika jamii nzima.

- Ubaguzi unaosababishwa na mtu kuambukizwa UKIMWI unajumuisha kupima ili kumwachisha mtu kazi au kutompandisha cheo, kufichua siri, au kukataa kutengeneza mazingira mazuri ya kazi kulingana na mahitaji ya wafanyakazi wenye UKIMWI.

- Haki ya msingi ya kutobaguliwa ni kanuni ya msingi ya Shirika la Kazi Duniani -ILO ambayo inaweza kutumika kulinda haki na heshima ya wafanyakazi na familia zao dhidi ya ukiukwaji wa haki zao kutokana na watu kujua au kuhisi kwamba ni waathirika wa virusi vya UKIMWI.

## Itikio la Shirika La Kazi Duniani

- Shirika la Kazi Duniani - ILO, linahamasisha mbinu ya kulinda haki za msingi za mfanyakazi katika kupambana na athari za UKIMWI katika ulimwengu wa kazi. Hii inahitaji kuwepo kwa ubinadamu na huruma, mfumo wa maadili mazuri na mfumo wa sera zitakazotumika kupambana na ubaguzi na hitaji la ulinzi wa jamii. Haki za msingi za wafanyakazi walioathirika ni pamoja na haki ya kufanya kazi, kupata mafunzo na kupandishwa cheo; haki ya kupata ulinzi wa jamii na mafao; haki ya kutunziwa siri kuhusu hali ya afya; pamoja na haki ya kupata kazi nyingine nzuri. Haki hizi za mahali pa kazi huzungumziwa katika Mikataba ya ILO, na kupewa uzito na Tamko la ILO juu ya Kanuni na Haki za Msingi katika Mahali pa Kazi, Mikataba mingine inayohusu swala la Afya na Usalama katika Mahali pa Kazi, pamoja na miongozo ya utekelezaji ya ILO iliyopo.

- ILO huchukulia ubaguzi wa watu wenye UKIMWI kama ukiukwaji wa haki za binadamu. Mkataba unaohusu ubaguzi katika sehemu za kazi kwa sababu ya UKIMWI ni mkataba Na. 111. Mikataba mingine inayohusu jambo hilo ni pamoja na: Mkataba Na. 158 kuhusu kuachishwa kazi; Mkataba Na. 155 kuhusu usalama na afya katika mahali pa kazi; Mkataba Na. 159 unaohusu kuwawezesha wafanyakazi kuishi katika mazingira mazuri ya kazi; na Mikataba Na. 97, 143 na 157 inayohusu makundi ya wafanyakazi wenye hatari kubwa ya kuambukizwa, kama vile wauguzi na wafanyakazi wanaosafiri mara kwa mara.

4, route des Morillons, CH-1211 Geneva 22, Switzerland, Website: www.oil.org Simu: (+41 22) 799 64 86, Fax: (+41 22) 799 63 49, Email: ILOAIDS@ilo.org
Kanda ya Africa Mashariki, S.L.P. 9212 Dar es Salaam, Tanzania. Simu: 255 22 21268821/4/6 Fax: 255 22 2126627 Email: daresalaam@ilo.org

Shirika la Kazi Duniani
Mpango wa Kimataifa unaohusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi

## Mwongozo wa ILO kuhusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi

- Mwongozo huu wa ILO, uliorekebishwa mwezi Mai, 2001, unahusu moja kwa moja athari za UKIMWI katika Ulimwengu wa kazi. Unatoa miongozo kwa serikali, waajiri na wafanyakazi na mashirika yao katika kuunda na kutekeleza sera na mipango katika ngazi za kitaifa na mashirika katika kukabiliana na UKIMWI.

- Mwongozo huo una kanuni kadhaa kama vile: kuziheshimu haki za msingi katika sehemu za kazi; ikiwa ni pamoja na kutokubaguliwa, kutambua kuwa UKIMWI ni suala la mahali pa kazi; usawa wa jinsia; majadiliano ya jamii; kutunza siri; na kutoa huduma na msaada kwa waathirika.

- Mwongozo unawahusu wafanyakazi wote walio katika sekta za umma na binafsi, rasmi na zisizo rasmi. Huhamasisha upatikanaji wa kazi zenye heshima na kuainisha wajibu wa serikali, vyama vya wafanyakazi na waajiri katika kudhibiti na kupunguza athari za UKIMWI katika mahali pa kazi.

- Kwa kuhamasisha serikali, waajiri na wafanyakazi na mifumo yao ya mitandao ya kupata habari, mwongozo utakuwa chombo cha kusaidia kulinda haki na hadhi ya wafanyakazi na familia zao pamoja na watu wote wanaoishi na UKIMWI.

4, route des Morillons, CH-1211 Geneva 22, Switzerland, Website: www.oil.org Simu: (+41 22) 799 64 86, Fax: (+41 22) 799 63 49, Email: ILOAIDS@ilo.org
Kanda ya Africa Mashariki, S.L.P. 9212 Dar es Salaam, Tanzania. Simu: 255 22 21268821/4/6 Fax: 255 22 2126627 Email: daresalaam@ilo.org